KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 13, Issue 1

5th Ramadhân 1432

5th Aug, 2011

YALIYOMO

HUKMU, ADABU NA SUNNAH ZA SAUM[Prt.3] 1 - 4

HUKMU, ADABU NA SUNNAH ZA SAUMU [Pt. 4]

Na: Sheikh Muhammad Saalih Al-Munajjid

(53) "Mtu yoyote mwenye kutapika bila ya kukusudia hatokuwa na haja ya kuilipa siku hiyo baadae, lakini yoyote mwenye kujitapisha kwa makusudi, itampasa ailipe siku hiyo baadae." (Ni hadeeth swaheeh iliyopokewa na at-Tirmidhee, 3/89). Mwenye kujitapisha kwa kujishindilia kidole ndani ya koo yake au kujikamua tumbo lake, au kunusa harufu yenye kutapisha, au kuangalia kitu kiwezacho kumtapisha, atawajibika kuilipa siku hiyo baadae. Iwapo atajisikiya kutapika, lakini mara tapishi likapote lenyewe, jambo hilo haliharibu saumu yake, kwa sababu hilo haliko chini ya uwezo wake, lakini iwapo tapishi litakuja kwenye mdomo wake kisha akalirudisha tena tumboni mwake, tendo hilo linaharibu saumu. Iwapo mtu atakuwa na maradhi ya tumbo, hatokuwa na haja ya kuzuiya tapishi lake, kwa sababu kufanya hivyo huwenda kukamletea madhara. (Majaalis Sharh Ramadaan, Ibn 'Uthaymeen, 67). Iwapo mtu atamiza kwa bahati mbaya kitu kilichokuwa kimesaki baina ya meno yake, au iwapo kitu hicho kilikuwa ni kidogo mno kiasi cha kwamba haielezeko iwapo kimebaki mdomoni mwake au alikitema, hiyo itahesabiwa kuwa ni katika sehemu ya mate yake na haiharibu saumu yake. Lakini lau kitu hicho kitakuwa ni kikubwa kinachoweza kutemwa, na afanye hivyo. Iwapo atakitema kitu hicho, hilo ni SAWA, lakini iwapo atakitafuna na kukila, hilo litaharibu saumu yake. Iwapo ataweza kukimumunya mdomoni mwake, sehemu yake au chote kizima, na kikawa na ladha ya nyongeza au utamu, inakuwa ni haraam kwake kukila kitu hicho. Iwapo kiini cha chakula hicho kitafika kwenye koo, hilo linaharibu saumu. Iwapo mtu atatema maji baada ya kusukutuwa, saumu yake haitoathirika na unyevu wowote wala majimaji yatakayobaki, kwa sababu haliko chini ya uwezo wake. Iwapo mtu anaugua maradhi ya kutokwa na damu za pua, saumu yake itakuwa sawa kwa sababu hili ni jambo asiloweza kulimiliki. (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/264). Iwapo atakuwa na kidonda kwenye magego yake (meno) au meno yake hutoa damu baada ya kutumia msuaki, haruhusiwi kuimiza damu hiyo, itambidi kuitema damu hiyo, ingawaje iwapo damu hiyo itapenya kwenye koo yake kwa bahati mbaya, wala yeye hakukusudia kufanya hivyo, haina haja ya kuwa na wasiwasi na jambo hilo. Vilevile iwapo tapishi litapanda kwenye koo yake na kisha likarudi chini kwenye tumbo lake pasi na yeye kukusudia kufanya hivyo, saumu yake itakuwa sawa (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/254).

JIPATIE KITABU CHA

"SAUMU YA MWEZI WA RAMADHÂN KAMA ILIVYOTEKELEZWA NA MTUME (صلى الله عليه وسلم)."

TUPIGIE SIMU KATIKA NAMBA HIZI:

+254- 0721473181 AU

+254-0727341779



HUKMU, ADABU NA SUNNAH ZA SAUM[Prt.3]

Ama kuhusu makamasi yatokayo kwenye kichwa (pua na maradhi ya Sinus) au makohozi yatokayo kwenye kifua kutokana na kukohoa au kusafisha kifua, iwapo yatamizwa kabla ya kufika mdomoni, hilo haliharibu saumu ya mtu, kwa sababu hilo ni tatizo alilonalo kila mtu, lakini litakapomizwa baada ya kuwa mdomoni, hilo linaharibu saumu. Ingawaje, iwapo litamizwakwa bahati mbaya, hilo halitoharibu saumu. Kuvuta pumzi na mvuke wa maji, kama iwezekanavyo kufanywa na watu wanaofanya kazi kwenye kampuni za uchungaji wa chumvi ya bahari, hakuathiri saumu. (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/276).

Ni jambo la makuruhu kuonja chakula bila ya sababu yoyote, kwa sababu jambo hilo linahatarisha kuharibika kwa saumu. Mfano wa hali zisizokuwa na budi ya kuonja chakula ni kina Mama kumumunya chakula cha kumpa mototo awapo hana njia nyengine ya kumlisha, kuonja chakula katika kuhakikisha yakwamba kiko sawa, na kuonja kitu unapokuwa katika hali ya biashara kutaka kuhakikisha. Imepokewa yakwamba Ibn Abbaas amesema: "Hapana makosa katika kuonja siki au kitu chochote ambacho mtu atakachokukinunua." (Imeorodheshwa kuwa hasan katika Irwa' ul-Ghaleel, 4/86; Tazama katika al-Fat-h, katika kusherehesha Baab Ightisaal al-Saa'im, Kitaab al-Siyaam).

(54) Kutumia Siwaak ni Sunnah kwa mtu yoyote aliyefunga nyakati zote za mchana, hata kama uko majimaji. Iwapo mwenye kufunga atatumia msuaki na akahisi mvuguto wa moto au ladha nyengine kutokamana na msuaki

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

huo na akamiza, au iwapo atautoa msuaki kutoka mdomoni mwake na akaupata na mate kasha akaurudisha mdomoni mwake na akamiza mate hayo, hilo halitoharibu saumu yake (al-Fataawa al-Sa'diyyah, 245).
Na ajiepusha na kitu chochote kiwezacho kumumunywa, kama vile msuaki wa kijani au msuaki wowote ulioongezwa ladha ya ziyada, kama vile limau au *Nanaa* (mint). Na ateme kutoka mdomoni mwake, vipande vyovyote vidogo vitokavyo kwenye msuaki, asivimize kwa kusudi, lakini iwapo atavimiza kwa bahati mbaya, hapatokuwa na madhara yoyote.

(55) Iwapo mwenye kufunga atapata ajali au atauguwa maradhi ya kutokwa na damu, au ataingiwa na maji au mafuta ya Petroli mdomoni mwake kwa bahati mbaya, jambo hili halitoiathiri saumu yake. Iwapo ataingiwa na vumbi, moshi au Nzi ndani ya mdomo wake kwa bahati mbaya, jambo hili vilevile halitoharibu saumu yake. Mambo/Vitu ambayo mtu hawezi kuyaepuka kuyamiza kama mtu kuyamiza mate yake this does not break his fast either. Things that one cannot avoid swallowing, like one's own saliva, au vumbi kutoka kwenye mashini ya kusaga Unga, haziharibu saumu. Iwapo mtu atakuwa na mate mengi katika mdomo wake kasha akayamiza kwa kukusudia, hili haliharibu saumu, kulingana na rai iliyosawa zaidi (al-Mughni by Ibn Qudaamah, 3/106). Lau mtu atatokwa na machozi yakaturuzika hadi kwenye koo yake, au lau mtu atajitia mafuta kwenye nywele zake au masharubu yake, au akatumia hina kisha akahisi ladha yake kwenye koo yake, jambo hilo halitoharibu saumu yake (Angalia kwenye Majmoo' al-Fataawa, 25/233, 25/245). Suala hili pia linahusiana na kupaka krimu (mafuta) yanayotumiwa kulainisha ngozi. Hapana makosa yoyote kwa kunusa harufu nzuri, kutumia mafuta mazuri au kujipaka krimu zenye kunukia vizuri na mfano wake. Hapana makosa kwa mwenye kufunga kutumia bukhoor (udi) maadamu hatoutumia kama ugoro (wa kunusa) (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/314). Kutotumia msuaki wakati wa mchana ni bora, na kuwachana nao hadi wakati wa usiku, kwa sababu ina nguvu sana (Al-Majaalis, Ibn 'Uthaymeen, p. 72).

(56) Ni bora kwa mfungaji, kwa usalama wake, asiumikwe (asifanyiwe hijaamah). Kuna ikhtilafu kubwa kuhusu suala hili. Ibn Taymiyyah ameonelea yakwamba mwenye kuumikwa anaharibu saumu yake (kuumikwa huharibu saumu lakini mwenye kuumika, saumu yake iko sawa).

(57) Uvutaji wa Sigara huharibu saumu ya mtu, na wala jambo hilo haliwezi kutumika kuwa ni udhuru wa mtu kutofunga. Itawezekanaje kwa madhambi kuchukuliwa kuwa ni udhuru?! (58) Mtu kujizamisha chini ya maji au kujifunika na tambara la maji kwa ajili ya kujiburudisha haiharibu saumu. Hapana makosa kwa mtu kujimwagia maji kichwani kwa ajili ya kupata burudiko kutokamana na joto au kiu. Kuogelea ni jambo lisilopendekezwa, kwa sababu huwenda kukamfanya mtu aharibu saumu yake (kwa kumiza maji). Iwapo kazi ya mtu inahusiana na kupiga mbizi kwenye maji na akawa na uhakika yakwamba hatopata maji kuingia ndani ya mdomo wake, basi hapana makosa na jambo hilo.

(59) Iwapo mtu atakula, au atakunywa au ataingiliana na mkewe kimapenzi, na huku akidhania yakwamba bado ni usiku, na mara akatambua yakwamba kumeshapambazuka, hapatokuwa na makosa hapo, kwa sababu aya imeeleza waziwazi yakwamba inaruhusiwa kufanya mambo hayo mpaka mtu awe na hakika yakwamba kumeshapambazuka. Amepokea 'Abdur-Razzaaq kwa isnaad iliyo swaheeh iliyotoka kwa Ibn Abbaas (رضي الله عنهما) yakwamba amesema: "Allaah amewaruhusu kula na kunywa maadamu kwenye fahamu zenu hamuna shaka yoyote." (Fath al-Baari, 4/135; vilevile hii ni rai ya Sheikh ul-Islaam Ibn Taymiyyah, Majmoo' al-Fataawa, 29/263).

(60) Iwapo mtu atavunja saumu yake, kwa kudhania yakwamba jua tayari limeshakutwa, na haliyakuwa bado halijatwa, itamlazimu ailipe saumu yake baadae (kulingana na wanavyuoni wengi), kwa sababu kimsingi bado ni mchana, na jambo la uhakika ulio na yakini haliwezi kukataliwa badala ya jambo lenye shaka (Rai ya Sheikh ul-Islaam ni kwamba haimpasi mtu aliye kwenye hali hiyo kuilipa siku hiyo). Iwapo alfajiri itaingia na mtu akawa na chakula mdomoni mwake, basi wameafikiyana mafuqahaa' yakwamba na akiteme chakula hicho, na saumu yake itakuwa sawa. Hukmu hii inafanana na ile hukmu ya mtu mwenye kula au kunywa kwa kusahau, kisha akakumbuka yakwamba amefunga - iwapo ataharakisha

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

TANGAZO LA DARSA ZA RAMADHÂN 2011/1432H

MASJID MAZRUI [KILA SIKU BA'DA SWALAAT ADH-DHUHR]

JUMATATU HADI JUMATANO / [Nawaaqidh ul-Islaam] / Ustadh Athman Bin Na'man

ALKHAMIS / [-] / Ustadh Sharrif

JUMAMOSI NA JUMAPILI / [AL-WAABIL AS-SWAYYIB] / Abu 'Abdur-Razzaq Haruna Rass.

DARSA ZA WANAWAKE MASJID MAZRUI NI KILA SIKU [ISIPOKUWA IJUMAA] KUANZIA SAA NNE ASUBUHI MPAKA SAA SITA.

MASJID KHAYRAAT [KIZIWI] [BA'DA SWALAAT ADH-DHUHR]

JUMANNE NA ALKHAMIS / [Ustaadh Muhammad Abdillah]

JUMATANO / [TAS-HEEL AL-AQEEDAH] / Abu Abdur-Razzaq Haruna Rass.

Unaweza kusikiliza Darsa hizi kwenye Mtandao (Internet)

Pal-Talk ⟹ All-Rooms ⟹ Religion & Spirituality ⟹ Islam ⟹ Callers to Tawheed ⟹ Swahili Duroos.

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

kukitema chakula au kinywaji kutoka mdomoni mwake, saumu yake itakuwa sawa.

HUKMU ZENYE KUHUSIANA NA SAUMU ZA WANAWAKE

(62) Mwanamke aliyefika umri wa kubaleghe, lakini akawa na haya nyingi sana kumueleza yoyote, kwahiyo akawa hafungi, itambidi atubie na azilipe siku alizokosa, pamoja na kumlisha maskini kwa kila siku aliyokosa, kuwa ni kama kitendo cha kulipa kafara kwa kucheleweshe saumu yake, na iwapo Ramadhân ifuatayo itafika na akawa hajalipa siku hizo. Hali yake ni kama ile ya mwanamke aliyefunga kwenye siku zake za ada kutokana na kuona kwake haya, na asizilipe baadae. Iwapo mwanamke hajui haswa ni siku ngapi aliwacha kufunga, na afunge mpaka apate uhakika yakwamba siku hizo alizoziacha ziwe zimelipika kutoka Ramadhân iliyopita, na kutoa kafara kwa kucheleweshe kufunga kwa kila siku aliyokosa. Anaweza kufanya hivyo wakati ule-ule wa kufunga au wakati mwengine, yote hayo kwa kutegemea analotaka kufanya. (63) Mwanamke na asifunge - isipokuwa katika mwezi wa Ramadhân - kama mumewe yuko nae pasi na ruhusa yake, lakini iwapo atakuwa ni msafiri, basi itakuwa haina neno.
(64) Mwanamke aliye kwenye heidh atakapo ona majimaji meupe - yanayotoka kwenye kizazi imalizikapo ada yake - alama ambayo wanawake huijua pindi watwahirikapo, itamlazimu awe na niya ya kufunga kuanzia usiku uliotangulia jana yake na afunge. Iwapo atakuwa hana wakati pindi ajuapo yakwamba, itamlazimu ajiingize kipande cha pamba au kitu mfano wake, na iwapo itatoka na kuwa swafi, itamlazimu kufunga, na iwapo ataanza kutokwa tena na damu, itamlazimu awache kufunga, emma damu hiyo ikiwa ni yenye kumwagika au ni ya vitone peke yake, kwa sababu inaharibu saumu maadamu inatoka wakati wa ada yake (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/154). Kama kukoma kwa damu kwa muda kutaendelea mpaka Maghrib, nae akawa amefunga kwa niya ya kutokea usiku wa jana, basi saumu yake inakuwa sawa. Iwapo mwanamke atajisikiya tumbo lake lakatwa na damu ya ada yake, basi saumu yake itakuwa sawa. lakini ikawa haitoki mpaka baada ya kuzama kwa jua, saumu yake itakuwa sawa na hatokuwa na haja ya kuilipa siku hiyo baadae. Iwapo ada ya mwanamke au damu yake za mazazi itakoma wakati wa usiku, na akatia niya ya kufunga, lakini alfajiri ikamjilia kabla ya kuweza kutekeleza Ghusl (kujitwahirisha), kulingana na wanavyuoni wote, saumu yake itakuwa sawa (al-Fath, 4/148)

(65) Iwapo mwanamke atajua yakwamba ada yake itamjilia kesho, na aendelee na niyab yake na afunge, na asivunje saumu yake mpaka ahakikishe kuiona damu.

(66) Ni bora kwa mwanamke aliye kwenye ada yake ya mwezi abakie katika hali yake na akubali alichoja'aliwa na Allaah kwa kutokula madawa ya kumzuiya kutoingia kwenye ada. Na atosheke na yale ambayo Allaah aliyomkadiria ya kuwacha kufunga wakati wa ada yake na kuzilipa siku hizo baadae. Hivi ndivyo ambavyo mama zao waumini na wanawake wa ki-Salaf. (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/151). Ya ziyada ni kwamba kuna ushahidi wa kitabibu kuthibitisha kuwa vitu vyingi vyenye kutumiwa katika kuzuiya kuingia kwenye ada vina madhara, na wanawake wengi wameathirika kwa kupoteza kawaida za masiku yao ya ada kutokana na utumiaji wa madawa hayo. Hatahivyo, iwapo mwanamke atafanya hivyo na akala kitu kuzuiya damu yake, kisha akafunga, hili ni SAWA.

(67) Istihaadah (isiyokuwa damu ya heidh) haina athari yoyote kuhusiana na kufaa kwa saumu.

(68) Iwapo mimba ya mwanamke itaharibika na kijusi kikaumbika au kikatambulika kwenye sehemu yoyote ya kiwiliwili, kama vile kichwa au mkono, damu yake hiyo itakuwa ni nifaas, hatahivyo iwapo atatokwa na kitu kama tone la damu ('alaq) au kipande ncha nyama kilichotafunwa kisichotambulika kwa umbile la kibinadamu, damu yake ni istihaadhah na itamlazimu kufunga, iwapo atakuwa na uwezo, vinginevyo anaweza kuvunja saumu yake akalipa siku hiyo baadae. (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/224).
Pindi atakapotwahirika baada ya kufanyiwa upasuaji wa kusafisha kizazi (D&C), ataweza kufunga. Wanavyuoni wamesema yakwamba kiini tete (embryo) huzingatiwa kuanza umbile lake baada ya siku 80 za mimba. Iwapo mwanamke atatwahirika kutokamana na nifaas kabla ya siku arubaini, atafunga na atekeleze ghusl ili aweze kuswali (al-Mughni ma'a al-Sharh al-Kabeer, 1/360). Iwapo damu itarudi tena ndani ya muda wa siku arubaini baada ya mazazi, na awache kufunga, kwa sababu hii bado ni nifaas. Iwapo damu itaendelea baada ya siku ya arubaini, na atiye niya ya kufunga na atekeleze ghusl (kulingana na wanavyuoni wengi), na damu yoyote baada ya siku ya arubaini itazingatiwa kuwa ni Istihaadhah (damu isiyokuwa ya ada) - isipokuwa iwapo itakutana na muda wake wa kawaida wa ada yake, ambao kwa mujibu wa hali ilivyo ni damu ya heidh.

Iwapo mwanamke mwenye kunyonyesha atafunga katika wakati mchana na akaona kitone cha damu katika wakati wa usiku, ingawaje alikuwa ametwahirika wakati wa mchana, saumu yake itakuwa sawa. (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/150)

(69) Kulingana na rai iliyo karibu na usawa, mwanamke mja mzito au mnyonyeshaji huzingatiwa kuwa kama mtu mgonjwa, kwahiyo anaruhusiwa kutofunga, na itambidi azilipe siku atakazokuwa amezikosa, ema atakapokuwa anahofia afya yake au ya mtoto wake. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم). "Allaah amemuondolea jukumu la kufunga mwanamke mja mzito na mwenye kunyonyesha." (Imepokewa na at-Tirmidhee, 3/85; amesema (hii ni hadeeth) hasan. Iwapo mwanamke mja mzito atafunga kisha apate damu, saumu yake itakuwa sawa, jambo hili haliathiri saumu yake hata kidogo. (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/225).

(70) Katika hali ya mwanamke aliyewajibika kufunga, iwapo mumewe ataingiliana nae katika mchana wa Ramadhân kwa makubaliano yao wawili, basi hukmu itakayomuathiri yeye vilevile itamuathiri mwenziwe. Iwapo, pengine yule mume atamlazimisha mke kufanya kitendo hicho, basi Yule mke na ajaribu awezavyo kumkatalia, na yeye

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 4)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

(mke), hatokuwa na haja ya kutoa kafara. Ibn 'Aqeel (رضي الله عنه) amesema: "Katika hali ya mume kufanya kitendo cha kumuingilia mkewe katika mchana wa Ramadhân haliyakuwa (Yule mke) amelala, (mke) hatokuwa na haja ya kutoa kafara." Lakini kwa njia ya kuondoa shaka, huyu mke nae pia ni bora ailipe siku hiyo baadae (Shaykh al-Islam Ibn Taymiyah (رحمه الله) alikuwa na rai yakwamba kitendo hicho hakikuharibu saumu yake kabisa). Mwanamke mwenye kujua yakwamba mumewe hawezi kujizuiya kabisa na ajiepushe kando nae na wala asijipambe na kujikwatua katika mchana wa mwezi wa Ramadhân . Wanawake ni lazima wazilipe saumu walizoziwacha katika mwezi wa Ramadhân , hata bila ya waume zao kujua. Si sharuti kwa saumu ya faradhi kwa mwanamke kupata idhini kutoka kwa mumewe. Ikiwa mwanamke ataanza kufunga saumu ya faradhi, haruhusiwi kuivunja saumu yake isipokuwa kwa sababu ya kisheriya. Mumewe haruhusiwi kumuamrisha kuvunja saumu yake atakapokuwa analipa siku aliyokuwa akidaiwa, haruhusiwi kuingiliana nae kimapenzi pindi atakapokuwa analipa siku yake, nae (huyu mke) haruhusiwi kumtwi'i (mume) kuhusiana na suala hilo. (Fataawa al-Lajnah al-Daa'imah, 10/353). Katika suala la saumu za Sunnah, mwanamke haruhusiwi kufunga saumu isiyokuwa ya faradhi pindi mumewe atakapokuwa nae pasi na ruhusa yake, kwa sababu ya hadeeth iliyopokewa na Abu Hurairah (رضي الله عنه) kulingana na alivyosema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Mwanamke haruhusiwi kufunga iwapo mumewe atakuwa nae isipokuwa kwa ruhusa yake." (Imepokewa na al-Bukhaari, 4793). Hatimae, haya ndiyo niliyoweza kuyaandika kuhusiana na mas'ala ya Saumu. Namuomba Allaah Atusaidie kumkumbuka Yeye, kumshukuru Yeye, na kumuabudu Yeye kisawasawa, na tuimalize Ramadhân yetu kwa kupata msamaha, na atuepushe na Moto. Twamuomba Allaah ambariki Mtume wetu Muhammad, na ahli yake na Maswahaba zake, na Awajazi kila la kheri.

SWALA YA TARAWEEH

All praise be to Allaah, and we send the prayers and salutations upon Allaah's Prophet , and upon his family and his companions and those who followed him, and upon those who follow his guidance. And then: Here are some useful papers collected on the subject of "Salaat at-Taraweeh," its rulings according to the Shari'ah, briefl y stated, hoping that Allaah may bring benefi t by it.

1. Its virtue: Its virtue has been mentioned in two Ahadeeth:

The fi rst: Narrated by Abu Hurairah, radia allaahu a'nhu, that the Prophet used to strongly encourage people to perform the Qiyaam in Ramadan, without vigorously ordering them to do so. Also, the Prophet said, "*Whosoever performs the Qiyaam (night prayers) of Ramadan with complete faith and expectation of the reward promised (by Allaah), his previous sins will be expiated.*"

The second: The hadith of Omar ibn Amr ibn Murra alJuhaneey, who said: A man from Qudaa'ah came to the Prophet and said: O Messenger of Allaah! Did you not see that if I were to bear witness that none is worthy of worship except Allaah, and that you are the messenger of Allaah, and I were to pray the fi ve prayers, and to fast the month, and to perform Qiyaam of Ramadan, and to give the Zakaat? To which the Prophet replied: "*Whosoever dies on this will be of the sid'eqeen wal shuhadaa' (the true believers and witnesses).*"

2. Its validity: The performing of Salaat at-Taraweeh in Jama'ah is valid, based on the Hadeeth of A'isha, radia allaahu a'nha, "*The Prophet left his home one night in the middle of the night, and he prayed in the Masjid. Men prayed following him in his prayer, and when the people awoke the following day, they spoke about it. So the next night an even larger number gathered, and followed him (i.e. – the Prophet) in his prayer, and when the people awoke the following day, they spoke about it, until the people's number in the Masjid was far greater the third night. So the Prophet went out again, and the people followed him in prayer. And when it was the fourth night, the Masjid was overfl owing with people, until he (i.e. the Prophet) came out for the morning prayer, and so when the Fajr prayer was completed he approached the people, utt ered the Shahada, and then said: "Surely it was not that I was unaware of your location, but rather I feared that it would be made compulsory on you, and then you would be incapable of performing it.*"" And until the Prophet died this remained the case. But, when the Prophet retuned to his Rabb, the Shari'ah became complete, and the fear was eliminated, and so the validity of its prayer (i.e. the Salaat-at-Taraweeh) in Jama'ah remained due to the elimination of the concern, as the concern and its corollary go hand in hand. And this Sunnah was revived by Omar ibn al Khatt aab, the rightly guided Khalifah as was related by Abd urRahman ibn AbdilQare', who said: "I went out with Omar ibn al Khatt ab, radi allaahu a'nhu, on a night in Ramadan to the Masjid, only to find the people in separate litt le groups, where a man would pray alone, or he would pray and only the old men would follow him in his prayer, and so Omar said: "I see that if I were to gather these people on a single reciter it would be ideal," and so he then decided and he gathered them behind Ubbay ibn Ka'ab. And then I went out with him on another night, and the people now were praying behind their reciter, Omar said: This is truly the best bida'a, and the one that they miss while sleeping is bett er than the one that they are performing, and the people used to perform the Qiyaam during the beginning part (of the night).

3. Its number of Rak'ahs:

The people have disagreed on the number
of its Rak'ahs, and the opinion that agrees

NENO LA BUSARA

"

KILA 'IBAADA AMBAYO MASWAHABA WA MTUME (صلى الله عليه وسلم) HAWAKUIFANYA, NA NYINYI MUSIIFANYE.

"

Hudhaifa ibn al-Yamani